SHULE YA SEKONDARI TLAWI,
S.L.P. 220,
MBULU-MANYARA.
……...

KUMB.NA TSS/J.INSTR/FORM V/VOL.1/07
SIMU YA MKONONI 0621068176/0785483040
JINA LA MWANAFUNZI
…….
SIMU YA MZAZI ……

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023**

Ninafurahi kukuarifu kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekuchagua kujiunga na Shule ya Sekondari Tlawi iliyoko Wilaya ya Mbulu Mkoa wa Manyara. Umechaguliwa kusoma mchepuo wa HGL/HGK na CBG. Shule itafunguliwa rasmi tarehe **……** unapaswa kuripoti kwa Makamu Mkuu wa Shule mara ufikapo shuleni ili usajiliwe. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ---------- baada ya hapo utapoteza nafasi hiyo.

Shule iko kata ya Tlawi, Tarafa ya Endagikot, Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Mkoa wa Manyara. Kwa usafiri wa Mbulu unaweza kutumia usafiri wa magari madogo aina ya cruser kutoka Arusha kupitia Magara au Karatu-Mbulu-Hydom, au utumie usafiri wa gari kubwa ya SANVIC toka Arusha- Haydom. Pia kutoka Singida usafiri upo wa mabasi makubwa aina HAJJ'S. Kutoka makao makuu ya wilaya ya Mbulu shule ipo kilomita 14 karibu na barabara iendayo haydom na kuna usafiri wa daladala kwenda Tlawi Nauli Tsh-1000/=.

Utakapo ripoti shuleni uwe na vifuatavyo:-

1. Barua ya maagizo (Joining instruction)
2. Vyeti vyako (original) na vivuli vya vyeti vya kidato cha nne (IV) Academic, Leaving na cheti cha kuzaliwa.
3. Cheti cha daktari (medical Examination Certificate) ambacho kimejazwa vizuri na Mganga mkuu wa hospitali ya Serikali na fomu ya makubaliano ya mzazi kumsomesha mwanao(Fomu zimeambatanishwa na barua hii)
4. Mto mmoja na foronya 2 za rangi ya blue bahari.
5. Neti ya mbu-mstatili
6. Blanketi 1 nzito
7. Taulo (1), nightdress, shuka yenye rangi ya blue bahari pea 1 kwa ajili ya ukaguzi na shuka 4 za rangi nyingine kwa ajili ya kulalia.
8. Mwavuli 1 buti ya matope kwa ajili ya shughuli za nje wakati wa mvua.
9. Sketi (2) za kazi rangi ya kijani kibichi mshono marinda kwa ajili ya kazi za nje na t- shirt rangi ya kijani.
10. Godoro ataikuta shuleni mwanafunzi aje na Tshs 20,000/= Uje nayo mkononi.
11. Vyombo vya chakula: - Sahani ya bati, (Aluminium) kikombe, bakuli na kijiko.
12. Traksuti 1 ya rangi ya blue bahari na mistari mweupe kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa

kujisomea.

13. Sare za michezo :- Track suti rangi ya bluu iliyokolea,tisheti ya njano na raba.
14. Viatu vyeusi vya kufunga na Gidamu visivyo na visigino virefu pea (2) na soksi nyeupe ndefu kwa ajili ya Darasani.
15. Sanduku la bati/chuma la kufunga kwa kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyako. .
16. Gharama ya matibabu ni juu ya mzazi na bima ndogo ni sh 6000

NB: Gharama nyingine ya dawa nje ya bima atagharimia mzazi, shuleni tunatoa huduma ya kwanza tu.

VIFAA VYA KAZI

1. Ndoo moja (1) yenye ujazo wa lita 20 kwa matumizi yake binafsi
2. Jembe lenye mpini imara kwa ajili ya kazi za shule.
3. Mopa 1,kwanja/fyekeo 1,ufagio wa chelewa 1,soft au hard broom 1 kwa ajili ya kufanyia usafi
4. Madaftari 10 (counter book Q4) na kalamu za kutosha.
5. Rula na mathematical set.
6. Scientific calculator.
7. Ream 1 size A4.
8. Dissectic kit kwa wanafunzi wa masomo ya Sayansi (CBG)

ADA NA MICHANGO YA SHULE

S/NO	FEDHA	MWAKA	MUHULA I	MUHULA II	MAONI
1.	Ada ya shule kwa mwaka	70,000/=	35,000/=	35,000/=	
2.	Gharama za tahadhari ambayo haitarudishwa	15,000/=	10,000/=	-	
3.	Kitambulisho na passport size (picha)	5,000/=	5,000/=	-	
4.	Uboreshaji wa Taaluma kwa mwaka	20,000/=	10,000/=	10,000/=	
6.	Ulinzi	20,000/=	10,000/=	10,000/=	
7.	Huduma ya kwanza na usafiri	20,000/=	10,000/=	10,000/=	
8.	Mpishi	20,000/=	10,000/=	10,000/=	
9.	Samani / ukarabati	18,000/=	18,000/=	-	
	JUMLA	**188,000/=**	**108,000/=**	**80,000/=**	

N:B Fedha zilipwe Benki kwa **Ac.No.41210011773** Bank ya **NMB**. Jina la Ac. **Tlawi Sec. School Development Account.** Fedha za matibabu zitapokelewa shuleni. Wenye kadi ya Bima ya Afya wajenazo shuleni.

Utakapofika shuleni unatakiwa kuwasilisha **"bank pay-in slip**" kwa mhasibu wa shule ili akuandikie stakabadhi ya malipo.

Kila mwanafunzi atagharamia mahafali mwaka kwa mwaka na uchapishaji wa cheti (ADVANCED LEAVING CERTIFICATE) mwaka wa mwisho wa masomo yake .

A. SARE YA SHULE KWA UJUMLA

Mwanafunzi anatakiwa ajishonee sare ya shule kwa kufuata Maelekezo na aina ya vitambaa vimeambatanishwa na fomu hii. Pamoja na mchoro wa mshono.

1. Sketi rangi dark blue pea mbili. Utajishonea, Rinda box kubwa nyuma na mbele.
2. Shati nyeupe yenye mikono mirefu pea mbili-Utajishonea / kujinunulia
3. Tai ndefu ya dark blue yenye mchirizi mweupe kama ulivyooneshwa kwenye mchoro.
4. Sweta rangi ya Dark Blue shingo V.
5. T-Shirt rangi ya damu ya mzee yenye colar form six (colar iwe nyeupe) ataikuta shuleni aje na Tsh 15,000/= mkononi.

B. SARE ZA SHULE KWA WANAFUNZI WA KIISLAMU

Wasichana wa madhehebu ya kiislamu wanapaswa kuvaa "HIJABU" kulingana na maadili ya dini yao na si vinginevyo:-

1. Suruali yenye rangi dark blue pea mbili. Utajishonea na si mlegezo wala model
2. Kanzu mbili nyeupe yenye mikono mirefu na hijabu rangi nyeupe -utajishonea. Kinyume na Maelekezo ya mashono hutopokelewa.

TANBIHI:
UREFU WA SKETI NI SENTIMETA 30 KUTOKA KWENYE GOTI

- Mwanafunzi hataruhusiwa kuja na nguo za nyumbani bali aje na vitu alivyoagizwa tu.
- Hutaruhusiwa kwenda bwenini kabla ya usajili kukamilika.
- Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.
- Soma vizuri sheria za shule na kuelewa kabla ya kusaini.
- Mwanafunzi haruhusiwi kutembelewa na mzazi au mgeni wake bwenini.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi. Ukikamatwa utafukuzwa shule


KOTI
SKETI
SURUALI
KANZU
TAI

Mwanafunzi anahitajika kuwa katika sare kamili awapo:-

(a) Masomoni, Darasani, atokapo nje ya shule kwa shughuli za kishule.

(b) Aendapo hospitalini.

(c) Safarini kuja shuleni na kwenda kwao.

MWISHO.

Kwa niaba ya Jumuiya ya Tlawi sekondari napenda kukukaribisha hapa shuleni, na kukutakia safari njema ya kuja shuleni.

……..

SULUO, FAUSTINI SANKA.

MKUU WA SHULE

0621 0681 76

Nakala

1. KATIBU MKUU,
   OR -TAMISEMI,
   S.L.P 9123.
   DODOMA.

2. MKURUGENZI WA MJI,
   HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU,
   S.L.P.164.
   MBULU- MANYARA.

A. SHERIA, TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE

1. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, anapoingia Darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
2. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kwa walimu, watumishi wasiowalimu, wageni na wanafunzi wenzake.
3. Mwanafunzi anapaswa kushiriki na kusaidia wenzake katika kazi.
4. Mwanafunzi analazimika kuheshimu na kuthamini aina zote za kazi shuleni na nje.
5. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-
   (a) Kuvuta sigara, kutumia madawa ya kulevya na kunywa pombe.
   (b) Vitendo vya wizi.
   (c) Kufuga ndevu, kucha ndefu, nywele ndefu, kupaka kucha rangi, wanja, rangi za midomo, na aina zozote za vipodozi, pia kuvaa hereni, shanga na bangili.
   (d) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima.
   (e) Kutembea na silaha.
   (f) Kugombana na makosa yoyote ya jinai.
   (g) Kuoa /kuolewa, uasherati kupata mimba, au kutoa mimba .
6. Mwanafunzi anapaswa kuitika mara na kukimbia aliko kiongozi anayemwita, pia kengele/filimbi iliapo akimbilie mstarini au anakotakiwa.
7. Mwanafunzi analazimika kuheshimu bendera ya Taifa, picha za Rais na Baba wa Taifa, Nembo yaTaifa (coat of Arms) wimbo wa Taifa.
8. Wanafunzi wanatakiwa kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote walipo.
9. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda nyumba za walimu isipokuwa kwa ruhusa maalum
10. Mwanafunzi aheshimu mahali pa kulia, ofisi za shule, mali yake binafsi na ya ummma.
11. Mwanafunzi anapaswa kutoa taarifa ya afya yake bila kuficha chochote.
12. Mwanafunzi anapaswa kunyoosha mkono juu na asimame anapouliza na kujibu maswali pia akae kimya awapo darasani wala asitoke bila ruhusa.
13. Mwanafunzi ni lazima awe msafi wakati wote na kuhakikisha kuwa mazingira ya shule ni masafi wakati wote.
14. Lugha itakayotumika shuleni kwa mawasiliano ni kiingireza
15. Utoro shuleni

B. IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA /WILAYA AU HOSPITALI NYINGINE ZINAZOTAMBULIKA NA MWANAFUNZI AJE NAYO NA KUMPA MKUU WA SHULE.

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Wilaya)
…… Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi)……..
Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana kuwa anayo/hanayo afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:-

(a) HALI YA MWILI:-

(i) Mapigo ya moyo ……
(ii) Haemoglobin (HB) ……
(iii) Kundi la damu (blood group) ……..
(iv) Mkojo (Urine) ……
(v) Kinyesi (stool) ……
(vi) Macho (Eye) …….
(vii) Masikio (Ear)……

Angalia:- Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (i) – (vii)

(b) MAGONJWA:-

*Amewahi/hajawahi/ana/hana/magonjwa yafuatayo:-

(a) Pumu ……..
(b) Kifua kikuu ……
(c) Kifafa …….
(d) Shinikizo la damu chini/juu ……
(e) Vidonda vya tumbo …….
(f) Maradhi ya zinaa ……
(g) Ukoma ……
(h) Mental illness (ugonjwa wa akili) ……
(i) Maradhi mengine yasiyotajwa hapo juu:-

……
……

……

SAHIHI NA MHURI WA DAKTARI /MGANGA

TAREHE ……

Kata lisilohusika.

C. **FOMU YA MAPOKEZI SHULENI – MAELEKEZO KUHUSU MWANAFUNZI**
SEHEMU A. (Ijazwe na mwanafunzi)
1. Jina la mwanafunzi (majina matatu)

……..

2. Uraia……..…

3. Tarehe ya kuzaliwa……

4. Shule anayotoka …….....

5. Tarehe ya kutoka shule hiyo …….....

SEHEMU B. (Ijazwe na mzazi / mlezi)

1. Jina la mzazi / mlezi (majina matatu) ……

2. Anwani ya mzazi/mlezi ……..

3. Mahali anapoishi ……...

4.Mawasiliano ya Mzazi/Mlezi(namba ya simu)……

5. Kazi ya mzazi/ mlezi ……

Mahali anapofanya kazi …….

5. Ndugu wawili wa karibu (wanaweza kuwa badala ya mzazi)

NB:Mwanafunzi atatembelewa Jumamosi ya mwisho wa mwezi

Jina la Ndugu wa I……Namba ya Simu……

Anuani yake: ……Uhusiano……..……

Jina la Ndugu wa II: …….Namba ya Simu……

Uhusiano wake : ……

TAREHE:…… SAHIHI YA MZAZI:……

D.MAKOSA YATAKAYOMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI.

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji wa bangi.
4. Makosa ya jinai.
5. Kupiga au kupigana.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.

E. FOMU YA MZAZI / MLEZI KUKUBALI WAJIBU WA KUMSOMESHA MWANAFUNZI.

Mimi …… …… wa kijiji cha ……
Kata ya ……Halmashauri ya……
Ambaye ni mzazi/mlezi wa ……...……
Anayeingia kidato cha …….. katika shule ya sekondari Tlawi najifungia wajibu huu kwa ajili ya kumsomesha mwanafunzi tajwa hapo juu mbele ya utawala wa kijiji changu hiki. Nimesoma barua ya kumwita shuleni sheria za shule na fomu zote zilizoambatishwa nimeelewa kila kitu na kuridhika. Pia najua nisipotimiza masharti yote mwanafunzi huyu hatopokelewa shuleni. Nakubali ahadi hiyo nikijua ni ahadi ambayo sitaweza kuikiuka bila hatua za kisheria zinazostahili kuchukuliwa dhidi yangu.

…… ……..

Sahihi ya mzazi au mlezi sahihi ya afisa mtendaji

Tarehe……. Tarehe ……

Namba ya simu……